**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

# MWONGOZO WA UFILISI WA VYAMA VYA USHIRIKA

***Imeandaliwa na:***
Tume ya Maendeleo ya Ushirika,
S. L. P. 201,
**DODOMA**

***TOLEO LA KWANZA APRIL, 2022***


## DIBAJI

Ufilisi wa Vyama vya Ushirika ni hatua muhimu katika kukamilisha zoezi la kufutwa kwa chama cha Ushirika. Chama cha Ushirika kinaanzishwa kwa malengo ambayo husaidia waanzishaji katika kuboresha maisha kwa kadri watakavyoona inafaa. Hata hivyo, pale ambapo chama kitashindwa, kwa sababu yoyote, ile kwa kadri zilivyoainishwa kwenye Sheria, kitalazimika kufutwa.

Chama, katika uhai wake, kinafanya mengi na hivyo kufutwa kwake kunapaswa kuzingatia yote kwa manufaa ya pande zote zilizoshiriki. Ufilisi, kwa mazingira yake ya kushughulikia chama kilichoshindwa, kunakuwa na changamoto nyingi kiasi kwamba baadhi ya ufilisi umekuwa ukichukua muda mrefu.

Mwongozo huu umelenga katika kufafanua taratibu za msingi za zoezi zima ili kuhakikisha kwamba wadau wote, hususan Maafisa Ushirika/Warajisi Wasaidizi wanaelewa zoezi hili muhimu na hivyo kuweza kusaidia katika kuhakikisha kuwa linafanyika vizuri na kwa wakati.

Ni matumaini ya Ofisi ya Mrajis kuwa mwongozo huu ukitumika vizuri utasaidia utekelezaji wa zoezi la ufilisi kufanyika kwa wakati na kupunguza migogoro kwa kuhakikisha kuwa mali na madeni ya Vyama vinavyofutwa zinapelekwa sehemu stahiki kwa mujibu wa Sheria.



Dkt. Benson O. Ndiege
**<u>MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA</u>**

## Yaliyomo

**DIBAJI** .... i
**Yaliyomo** .... ii
**SEHEMU YA KWANZA** .... 1
**UTANGULIZI** .... 1
**1.1 Mamlaka ya Mrajis** .... 1
**1.2 Uteuzi wa Mfilisi** .... 2
**1.3 Sifa na Maadili ya Mfilisi** .... 2
**1.4 Maadili ya Mfilisi (*Code of Conduct of Liquidator*)** .... 3
**1.5 Mamlaka ya Mfilisi** .... 3
**SEHEMU YA PILI** .... 5
**UTARATIBU WA UFILISI** .... 5
**2.1 Uhakiki wa Madai na Madeni** .... 8
**SEHEMU YA TATU** .... 9
**UTUNZAJI WA HESABU NA UTOAJI WA TAARIFA YA UFILISI** .... 9
**3.1 Hesabu za Ufilisi** .... 9
**3.2 Gharama za Mfilisi-** .... 9
**SEHEMU YA NNE** .... 10
**MATUMIZI YA FEDHA ZA UFILISI** .... 10
**SEHEMU YA TANO** .... 11
**UHITIMISHWAJI WA ZOEZI LA UFILISI** .... 11
**5.1 Matumizi ya Mali ya Ufilisi** .... 11
**5.2 Utunzaji wa Vitabu baada ya Ufilisi** .... 11
**SEHEMU YA SITA** .... 12
**HITIMISHO** .... 12

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

Vyama vya Ushirika vinasajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake za mwaka 2015. Sheria imetoa maelekezo ya jinsi ya kusajili, kuendesha, kusimamia na hatimaye kufuta pale ambapo panatokea ukiukwaji kwa sababu mbali mbali kama zilivyofafanuliwa katika sehemu ya kumi na mbili (xii) ya Sheria ya Vyama vya Ushirika. Chama cha Ushirika kikishafutwa kwa mujibu wa Sheria ndipo zoezi la ufilisi linapoanza.

Ufilisi wa Vyama vya Ushirika ni zoezi la kukamilisha hatua za ufutaji wa Chama cha Ushirika baada ya uhai wa chama hicho kusitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika kifungu cha 103. Ufilisi unahusisha upataji wa taarifa mbalimbali za Chama kilichofutwa kuhusu Mali na madeni ya Chama. Taarifa hizo zitasaidia kukusanya madeni na kuuza mali za chama ili kulipa madeni mbalimbali.

Kwa mujibu wa kifungu cha 99, Mrajis akijiridhisha kuwa chama kimekiuka Sheria ya Vyama vya Ushirika kifungu cha 100 na kustahili kufutwa, atafuta usajili wa chama kwa kutoa amri kwa maandishi kuhusu kusudio hilo. Chama, kwa upande wake, kitakuwa na nafasi ya kukata rufaa kwa mujibu wa kifungu cha 101, na pale ambapo itathibitika uhalali wa kufuta, chama kitafutwa na mchakato wa ufilisi kuanza.

Aidha, ufilisi wa chama utafanyika kwa mujibu wa kifungu cha 99: mara baada ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika kufanya uchunguzi kwa mujibu wa kifungu namba 91; wanachama zaidi ya robo tatu kuwasilisha maombi ya chama kufutwa; ukiukwaji wa vifungu namba 96 na 98 vya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013; chama kushindwa kuendesha shughuli zake ndani ya miezi sita au Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kushindwa kuwasilisha hesabu zilizokaguliwa kwa mujibu wa kanuni za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

Chama, katika uhai wake, kinafanya shughuli mbali mbali na kujipatia mali na vile vile kujilimbikizia madeni inapobidi na yote hayo yatahitaji kukusanywa na kulipwa; na hivyo kuwa na umuhimu wa zoezi la ufilisi.

Ufilisi huanza kwa kuchambua hali ya mali na madeni ya chama kilichofutwa, na kuweka utaratibu wa kukusanya na kulipa kwa mujibu wa Sheria ili hatimaye chombo hiki kilichokuwa na uhai kwa mujibu wa Sheria shughuli zake zihitimishwe kwa mujibu wa Sheria.

## 1.1 Mamlaka ya Mrajis

Mrajis, kwa kuzingatia sehemu ya kumi na mbili (xii), kifungu cha 100; amepewa mamlaka ya kufuta chama; na kwa mujibu wa kifungu cha 103, kuteua mtunzaji mali (*custodian*) ambaye

atakuwa na jukumu la kushikilia na kutunza kwa muda mali hadi mfilisi atakapoteuliwa. Mrajis, kwa mujibu wa kifungu cha 103(b), atawajibika kuteua mfilisi ndani ya siku 40 tangu kufutwa kwa Chama cha Ushirika.

### 1.2 Uteuzi wa Mfilisi

Mrajis wa Vyama vya Ushirika, ndani ya siku arobaini (40), atateua mtu mwenye sifa za kuwa mfilisi wa mali na madeni ya chama kilichofutwa. Mrajis atawajibika kutangaza kwenye gazeti la serikali, jina la mfilisi aliyeteuliwa. Mfilisi atapewa maelekezo ya jinsi ya kutekeleza jukumu hilo pamoja na muda wa kufanya kazi hiyo.

Mrajis, kwa kuzingatia kifungu cha 103 (3), amepewa mamlaka ya kupanga muda wa kufanya ufilisi katika Chama cha Ushirika. Hivyo, kwa mwongozo huu, anaelekezwa kuwa muda wa ufilisi utakuwa ndani ya miezi ishirini na minne tangu tarehe ya kufutwa kwa chama hicho.

Mrajis, katika barua ya uteuzi, anaweza kuweka ukomo au zuio kwenye mamlaka ya mfilisi kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika kifungu cha 104, au maelekezo hayo yanaweza yakatolewa baadaye au vinginevyo, na atakuwa na mamlaka juu ya mfilisi.

Iwapo hataridhishwa na utendaji wa kazi wa mfilisi, Mrajis ataweza kufuta uteuzi wa mfilisi huyo wakati wowote pasipo kutoa sababu na kumteua mfilisi mwingine. Mfilisi akifutiwa uteuzi atapaswa kukabidhi mali, nyaraka na kumbukumbu zote zinazohusiana na chama kilichofutwa kilichopo kwenye ufilisi kwa mfilisi atakayeteuliwa au kwa mtu yeyote atakayeteuliwa na Mrajis kwa madhumuni hayo. Taarifa ya makabidhiano itapaswa kuandaliwa katika nakala tatu na kutiwa saini na mfilisi anayekabidhi na mfilisi/mtu anayekabidhiwa na nakala moja ya taarifa hiyo kutumwa kwa Mrajis.

### 1.3 Sifa na Maadili ya Mfilisi

Kwa mujibu wa kifungu 103(b), mfilisi anatakiwa awe mwenye uwezo wa kutekeleza jukumu la ufilisi. Kwa kuzingatia Mwongozo huu, mrajis anaelekeza kwamba ili kutekeleza majukumu ya ufilisi ipasavyo, mfilisi anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(i) Kwa upande wa Vyama vya Ushirika vya msingi, awe na angalau kiwango cha chini cha elimu ya uhasibu katika ngazi ya astashahada au stashahada kwa kuzingatia ukubwa wa chama husika; na

(ii) Kwa upande wa Vyama vikuu vya Ushirika, Miradi ya Ushirika, Benki za Ushirika na Shirikisho la Vyama vya Ushirika, awe na angalau elimu ya uhasibu katika ngazi ya shahada, CPA (T).

TANBIHI: Mfilisi ata takiwa kutumia mwanaSheria katika kutekeleza baadhi ya majukumu yatakayo hitaji taaluma hiyo na kwa upande wa migogoro kutumia wasuluhishi kwa kuzingatia mazingira ya chama husika.

Mfilisi asiwe Mrajis au Mrajis msaidizi, ili kuondoa mgongano wa majukumu na uwajibikaji.

## 1.4 Maadili ya Mfilisi (*Code of Conduct of Liquidator*)

Mfilisi anapaswa kuwa mtu mwenye kuzingatia utendaji mzuri ili kuepuka vitendo vya rushwa; awe mwaminifu, muadilifu na anayewajibika.

Ni jukumu la Mrajis kuteua mtu mwenye sifa na weledi atakayeweza kuifanya kazi hii kwa usahihi kulingana na muda uliopangwa kwa mujibu wa mwongozo huu.

Mfilisi atatakiwa kuwa na hati ya makabidhiano ya kumbukumbu zote za chama kinachofilisiwa kati yake na Mtunzaji (*Custodian*) aliyeteuliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika kabla ya kuteuliwa kwa mfilisi. Hati hiyo itaonesha orodha ya mali (zinazohamishika na zisizohamishika) na madeni, hati Miliki za mali za chama, na hati za udhamini za wadaiwa wa chama.

Baada ya kukabidhiwa kumbukumbu kutoka kwa Mtunzaji (Custodian), mfilisi ataanza shughuli ya ufilisi kwa maelekezo ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika na kwa mujibu wa barua ya uteuzi wake (mfilisi) kutoka kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika**.**

Kwa kuzingatia mwongozo huu, mfilisi, mara baada ya kuteuliwa ndani ya siku 7, atapaswa kuandaa na kuwasilisha kwa Mrajis, mpango kazi wa namna atakavyotekeleza majukumu yake kwa ajili ya kuidhinishwa.

Sambamba na kazi nyingine za ufilisi, mfilisi atawajibika kufanya uthaminishaji wa mali (zisizohamishika na zinazohamishika) baada ya kupata idhini kutoka kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika na kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

## 1.5 Mamlaka ya Mfilisi

Mfilisi, kwa mujibu wa kifungu cha 104, ana mamlaka ya kutekeleza majukumu mbalimbali chini ya uongozi na usimamizi wa Mrajis. Majukumu ya mfilisi ni pamoja na:

(i) Kufungua mashtaka na kutoa utetezi katika kesi na mienendo mingine ya kiSheria kwa jina lake au jina la ofisi, na kufika mahakamani binafsi kama mdai au mdaiwa kwa niaba ya chama;
(ii) kuwasilisha migogoro inayohusiana na ufilisi kwa wasuluhishi;

(iii) kuweka viwango vya michango itakayolipwa na wanachama au waliokuwa wanachama na mali zilizo mikononi mwa wasimamizi wa mirathi ya waliokuwa wanachama wa chama kinachofilisiwa;
(iv) kubainisha na kuchunguza madai yote dhidi ya chama kwa mujibu wa Sheria na kuangalia vipaumbele vya wadai kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6. ya mwaka 2013, kifungu cha 113;
(v) kuweka kiwango cha gharama za ufilisi kwa uwiano, na kuonyesha nani atalipwa na nani atalipa;
(vi) kupitia na kuchunguza madai ya chama kwa wadaiwa wa chama kinachofilisiwa;
(vii) kuchukua na kumiliki vitabu vya hesabu, kumbukumbu zote za mali na madeni ya chama; na
(viii) kutoa maelekezo kuhusu ukusanyaji na usambazaji wa mali za chama na matumizi ya vitabu na nyaraka za chama, kama atakavyoona inafaa, kwa madhumuni ya kukamilisha shughuli za ufilisi wa chama;

Kwa mujibu wa kifungu Na. 141, mfilisi aliyeteuliwa ana mamlaka ya kumtaka shahidi kuhudhuria na kutoa nyaraka/vielelezo vyote kwa namna ile ile inavyotekelezwa kwenye kesi iliyoko mahakamani chini ya Sheria "*civil procedure code*" (CPC)

Vile vile, taratibu zinapaswa kutoa nafasi ya rufani kwenye mahakama ya hakimu mkazi kwenye eneo ambalo chama kipo. Mfilisi

## SEHEMU YA PILI

## UTARATIBU WA UFILISI

Ufilisi wa Vyama vya Ushirika unazingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013. Kwa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo na Benki za Ushirika, utazingatia Sheria ya Ushirika na baadhi ya taratibu kwa mujibu wa '*Banking and Financial Institution Act*.'

Benki ya Ushirika, kwa mujibu wa Sheria ya BAFIA, inaweza kufilisika kwa ridhaa ya wanahisa kwa idhini ya Benki Kuu ya Tanzania (Bank of Tanzania - B.O.T), ilimradi ufilisi huo utaonesha kwamba benki iliyoamua kufilisiwa ina uwezo wa kulipa amana na madai ya wadai. Ufilisi wa benki ya Ushirika unashirikisha pande mbili: Mrajis kufuta Usajili wa Benki kama Chama cha Ushirika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ambapo Mrajis hufuta usajili wa benki ya Ushirika, na hitimisho la ufilisi; na Benki kuu kuondoa/kufuta leseni ya biashara na kusimamia shughuli nyingine za Ufilisi wa Benki kwa mujibu wa BAFIA.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika hupokea taarifa ya ufilisi wa benki iliyokaguliwa na mkaguzi wa kujitegemea na kupeleka kumbukumbu za ufilisi kwenye Ofisi ya nyaraka za Taifa (*archived*).

Kwa upande wa chama cha Ushirika wa Akiba na mikopo, kitafilisiwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, vifungu Na. 99-120. Vile vile, kwa mujibu wa *Banking and Financial Institution Act*, Benki kuu itawasiliana na Mrajis wa Vyama vya Ushirika ili taratibu nyingine za ufilisi wa chama cha Akiba na Mikopo zifanyike kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika.

Kwa ujumla, katika kutekeleza jukumu la ufilisi kuna taratibu zinazopaswa kufuatwa kabla na baada ya zoezi kuanza katika kila chama kinachofilisiwa, isipokuwa kwa Vyama vya Ushirika vya kifedha "SACCOS" na Benki za Ushirika.

Kwa chama ambacho hakina mali za kufilisi, Mrajis anaweza kukifuta chama hicho moja kwa moja bila kufanya Ufilisi.

Ufilisi utafuata taratibu zifuatazo:

(a) Mara baada ya Chama cha Ushirika kufutwa, Mrajis ataandaa na kutangaza (kwa njia anazoamini ni muafaka) notisi itakayotaka madeni yote yanayokihusu chama cha Ushirika kinachofilisiwa, kuwasilishwa kwake au kwa mtu ambaye atakuwa amemteua kama Mhifadhi na/au Mfilisi ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kutangazwa notisi hiyo. Kutokana na kutolewa kwa tangazo hilo, itaaminika kuwa kila mdai ambaye ameandikwa kwenye kumbukumbu za chama kilichofutwa ametaarifiwa;

(b) Mfilisi ataweka muda ambao kila mdai atapaswa kuthibitisha madeni au madai yake. Aidha, atatoa tangazo kwenye gazeti la serikali na ataweza pia kutangaza kwenye magazeti mengine akiufahamisha umma kuhusu jukumu lake na wajibu wa kila mlengwa katika chama hicho kuthibitisha madai yake; akitoa rai kwa wale ambao hawatafanya hivyo kwamba madai au madeni yao hayatafanyiwa kazi.

Iwapo hakuna madeni au madai ambayo yatakuwa yamewasilishwa kwa mfilisi katika kipindi cha ndani ya siku sitini tangu kutolewa kwa agizo la kufutwa kwa chama cha Ushirika husika, mfilisi anapaswa kukataa kupokea na kuyafanyia kazi madeni au madai yatakayowasilisha baada ya hapo;

(c) Mara baada ya chama cha Ushirika kufutiwa Usajili, Mfilisi atachukua udhibiti wa vitabu vya chama cha Ushirika kilichofutwa pamoja na mali zake zote kwa minajili ya kufunga shughuli zake. Mfilisi atapaswa kuandaa kwa haraka, taarifa ya shughuli za chama hicho ambazo zitajumuisha taarifa zifuatazo;

(i) Mali na madeni ya chama kilichofutwa zikiwemo; mali za kudumu (zinazohamishika na zisizo hamishika), wadaiwa mbalimbali (walio na dhamana na wasio na dhamana), samani mbalimbali, Mahujudi/bidhaa ghalani (*Stock*), Fedha (Mkononi na Benki), kama zipo, na Dhamana zinazobadilishika (*Negotiable Securities*) zinazomilikiwa na chama hicho kama zipo;
(ii) Dhima; zikiwemo za muda mrefu ambazo ni mtaji utakaojumuisha Hisa za Wanachama, malimbikizo mbalimbali, ziada za biashara, mikopo ya muda mrefu, madeni ya muda mfupi kama vile wadai.
(iii) Majina, anuani na shughuli za wadeni wa chama kilichofutwa wakiainishwa kwa utofauti kati ya kiasi cha madeni yaliyowekewa dhamana na ambayo hayajawekewa dhamana;
(iv) Madeni ambayo Chama cha Ushirika kilichofutwa kinadaiwa na majina, makazi na shughuli za watu wanaodaiwa na chama hicho, na kiasi kinachodaiwa; na
(v) Taarifa nyinginezo kadiri itakavyoelekezwa na Mrajis.

(d) Taarifa inayotakiwa kuandaliwa katika (iii) hapo juu lazima itokane na kumbukumbu za chama cha Ushirika kilichofutwa. Ionyeshe taarifa za ukaguzi za miaka mitatu ya nyuma, na maelezo yatakayotolewa na waliokuwa Wajumbe wa Bodi, aliyekuwa Mtendaji Mkuu, Mhazini au Afisa mwingine wa Chama cha Ushirika kilichofutwa wakati zoezi la Ufilisi lilipokuwa linaanza. Mfilisi atapaswa kuchukua maelezo ya maandishi kutoka kwa watendaji wa chama hicho cha Ushirika wakiwa katika kiapo. Mfilisi atapaswa kuikamilisha na kuiwasilisha taarifa hiyo kwa Mrajis katika kipindi kisichozidi siku ishirini na moja tangu tarehe ya uteuzi wake au ndani ya muda utakaoongezwa na Mrajis; lakini ambao

hautakuwa zaidi ya siku arobaini na tano tangu tarehe ya amri ya kufutwa kwa Chama cha Ushirika husika;

(e) Mfilisi atabainisha hali ya kila mwanachama na michango yao kwenye mali za chama;

(f) Mfilisi ataandaa orodha ikionesha majina ya wanachama waliopo na wanachama wa zamani pamoja na warithi wao; ikionesha kiasi ambacho kinatarajiwa kupatikana kutoka kwa kila mmoja kama mchango kwa mujibu wa (v) hapo juu. Katika kuandaa orodha hiyo, mfilisi atapaswa kutofautisha majina ya wachangiaji ambao watachangia kama wajibu wao na wale ambao watachangia kama wawakilishi/warithi wa Wanachama. Katika kipindi chote baada ya uteuzi wake, mfilisi ataweza kuagiza mchangiaji yeyote ambaye yupo kwenye orodha iliyomo kwenye agizo, Wakfu, Benki, Wakala au Afisa wa chama cha Ushirika mfu kulipa, kupeleka, kukabidhi au kuhamisha kwa mfilis, bila kukawia; fedha, mali, vitabu au nyaraka zilizomo katika himaya yake na ambazo kwa ushahidi uliopo ni mali ya chama cha Ushirika kilichofutwa;

(g) Mfilisi atapaswa kuwasilisha kwa Mrajis agizo aliloliandaa katika (vi) hapo juu kwa ajili ya mapitio na idhini. Katika mapitio yake, Mrajis ataweza kulifanyia marekebisho agizo au kulirejesha kwa mfilisi kwa ajili ya kufanya uchunguzi zaidi au hatua nyingine na baadaye kujumuisha marekebisho hayo na kuliwasilisha tena kwa Mrajis kwa ajili ya idhini;

(h) Nakala ya agizo kama lilivyoidhinishwa na Mrajis, likiambatishwa, pale itakapowezekana, na orodha ya mali za kila mwanachama au mwanachama wa zamani ambaye amri (*decree*) ya kuchangia inapaswa kukaziwa dhidi yao, haina budi kuwasilishwa mahakamani kwa ajili ya kukaziwa;

(i) Iwapo amri haitatekelezwa kwa mujibu wa (viii) ili mfilisi akusanye kiasi cha fedha kilichokadiriwa dhidi ya mwanachama au wanachama, mfilisi atatakiwa kuandaa agizo/maagizo la/ya ziada dhidi ya mwanachama/wanachama kwa kiwango cha dhima ya kila deni la chama cha Ushirika kilichofutwa hadi kiasi chote anachodaiwa wanachama kitakapokusanywa kwa ukamilifu na utekelezwaji wa maagizo hayo utakuwa kwa utaratibu uleule;

(j) Fedha zote ambazo zitakuwa chini ya udhibiti wa mfilisi zitatakiwa zitunzwe benki katika akaunti ya hundi ambayo itafunguliwa na mfilisi kwa jina la Chama cha Ushirika kilichofutwa kilichopo chini ya ufilisi. Fedha za ufilisi zitakazopokelewa zitapaswa kupelekwa kwenye akaunti ya ufilisi ndani ya saa ishirini na nne tangu kupokelewa kwake. Malipo yote katika akaunti ya ufilisi hayana budi yapate kibali cha Mrajis ndipo hundi ziweze kuandikwa na mfilisi kwa maslahi ya walipwaji. Mfilisi ataweza kuomba kwa Mrajis kuruhusiwa kutunza kiasi fulani cha fedha taslimu mkononi (*Petty Cash*) kwa ajili ya kugharimia mahitaji madogo madogo ya shughuli za ufilisi; na

(k) Mtu yeyote ambaye kwa udanganyifu atadai kuwa mdeni au mdai wa Chama kilichofutwa atakuwa anatenda kosa kwa mujibu wa Sheria ya makosa ya Jinai, na atapelekwa mahakamani kwa maombi ya mfilisi..

### 2.1 Uhakiki wa Madai na Madeni

Baada ya tangazo, wadai na wadaiwa wote watawasilisha kwa mfilisi ushahidi wa madai yao kwa ajili ya uhakiki ndani ya siku zisizozidi sitini kama zilivyotangazwa na mfilisi.

Endapo ikatokea katika mazingira ambayo dai lilithibitishwa na mdai lakini halikuweza kulipwa na mfilisi kutokana na mdai kutoonekana au kwa sababu nyingine yeyote, kiasi cha fedha kinacholingana na kiwango cha dai hilo ambalo halijalipwa kitapaswa kuwekwa kwenye akaunti kwa jina la Mrajis na zitabaki na uhalali wa kulipwa kwa mdai kwa kipindi kisichozidi miaka miwili tangu tarehe ya kutimizwa kwa agizo la kufutwa kwa usajili wa chama cha Ushirika husika;

Baada ya hapo, kiasi hicho cha fedha kitachukuliwa kama ziada ambayo itatumika katika shughuli za maendeleo ya Ushirika.

## SEHEMU YA TATU

## UTUNZAJI WA HESABU NA UTOAJI WA TAARIFA YA UFILISI

### 3.1 Hesabu za Ufilisi

Ili kuhakikisha kwamba hesabu na taarifa za chama kilichofutwa zinaandaliwa ipasavyo, mfilisi atapaswa kufanya yafuatayo;

(a) Kuandaa makisio ya mapato na matumizi ya shughuli za ufilisi kwa mwaka na kuyawasilisha kwa Mrajis kwa ajili ya kuidhinishwa. Kutunza vitabu na hesabu za ufilisi kwa kadiri itakavyoelekezwa na Mrajis; na

(b) Kuandaa na kuwasilisha kwa Mrajis taarifa ya utekelezaji wa kazi za ufilisi kwa kila robo mwaka, taarifa ya mwaka na taarifa ya mwisho ya ufilisi. Taarifa hiyo itajumuisha yafuatayo:

 (i) Urari;
 (ii) Mapato na matumizi; na
 (iii) Taarifa ya usuluhishi wa hesabu za akaunti za benki.

Kutoa hati za malipo, hesabu zake zote, mikataba, nyaraka mbalimbali na maelezo mengine yatakayohitajika kwa ajili ya kukaguliwa.

Mrajis atapaswa kuelekeza vitabu na hesabu za mfilisi kufanyiwa ukaguzi wa kawaida kwa kila robo mwaka; ambao utafanywa na Maafisa Ushirika wakaguzi na wakaguzi wa nje kwa vipindi vya kila mwaka pale ambapo ufilisi utakuwa umechukua zaidi ya mwaka; na pale ambapo utakuwa umechukua chini ya mwaka, Mkaguzi atakagua kwa kipindi kilekile cha ufilisi ambacho ni chini ya mwaka. Taarifa za ukaguzi utakaofanyika zinapaswa kuwasilishwa kwa Mrajis, na mfilisi kupatiwa nakala kwa ajili ya kuandaa majibu ya hoja zilizobainishwa. Mfilisi atapaswa kuandaa majibu ya hoja za ukaguzi wa kawaida na kuyawasilisha kwa Mrajis; na kwa upande wa taarifa ya ukaguzi wa nje, mfilisi atapaswa kuandaa majibu ya hoja na kuyawasilisha kwa Mkaguzi wa Nje hadi zitakapojitosheleza. Mkaguzi wa Nje atapaswa kumtaarifu Mrajis juu ya hali ya utekelezaji wa utoaji wa majibu ya hoja zake pamoja na marekebisho yaliyofanywa kwenye kasoro zilizoibuliwa na taarifa yake.

### 3.2 Gharama za Mfilisi-

Mfilisi anatakiwa kuwa na bajeti ya ufilisi ambayo itazingatia mpango kazi na ambayo itaidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika. Bajeti ya ufilisi, itajumuisha gharama za uthaminishaji wa mali za kudumu zinazohamishika na zisizohamishika, gharama za uendeshaji wa ofisi ya mfilisi, posho/mshahara wa mfilisi, gharama za benki, gharama za vitabu na karatasi,

mishahara/posho za wasaidizi wa mfilisi, gharama za umeme, gharama za upangaji kwa ajili ya ofisi ya mfilisi n.k.

Mfilisi ataendelea kufuatilia wadeni wa chama kwa njia mbalimbali zilizoidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

## SEHEMU YA NNE

## MATUMIZI YA FEDHA ZA UFILISI

Mfilisi atahakikisha kuwa anakusanya fedha kutoka kwa wadaiwa wote wa chama kinachofilisiwa, fedha kutokana na mauzo ya mali zinazohamishika na zisizohamishika, riba kutokana na fedha zilizoko kwenye dhamana Benki,dhamana (*Bonds*) za Serikalini, Vitega uchumi, misaada kutoka kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Wafadhili wengine wa shughuli za ufilisi. Fedha hizo zitakatiwa risiti au vitabu vya mapokezi ya fedha na kisha kuwasilishwa Benki kwenye Akaunti ya Mfilisi.

Fedha hizo za makusanyo zitatumika kwa kuzingatia vipaumbele, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika kama ifuatavyo:

(i) Wadai wenye dhamana;
(ii) Serikali kwa kodi mbalimbali zikiwemo, kodi za mapato, “Capital gains tax” kwenye uuzwaji mali za kudumu na zinazohamishika;
(iii) Watumishi wa chama mishahara waliokuwa wanadai chama;
(iv) Mifuko ya hifadhi ya Jamii kwa michango mbalimbali;
(v) Wadai wengine ambao hawana dhamana; na
(vi) Gharama za Ufilisi kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

Malipo yote yatatakiwa kupata kibali cha Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa mujibu wa bajeti na mpango wa malipo kwa madai yaliyoidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

Baada ya kukusanya madeni yaliyopaswa kulipwa kwa chama hicho na kupokea michango kutoka kwa wanachama na wanachama wa zamani na kulipa madeni, mfilisi atakamilisha shughuli za ufilisi na kuwasilisha taarifa ya mwisho kwa Mrajis.

## SEHEMU YA TANO

## UHITIMISHWAJI WA ZOEZI LA UFILISI

### 5.1 Matumizi ya Mali ya Ufilisi

Mali ambazo hazikuuzika katika mchakato wa Ufilisi kama zitakavyooneshwa kwenye taarifa ya mwisho ya mfilisi wa chama cha Ushirika kilichofutwa ambacho ufilisi wake umekamilika, zinaweza kugawanywa na Mrajis miongoni mwa Vyama vya Ushirika vilivyopo kwenye eneo la Chama kilichofutwa. Aidha, mali hizo zitapaswa kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

### 5.2 Utunzaji wa Vitabu baada ya Ufilisi

Kwa mujibu wa kifungu Na. 120, Mfilisi atawajibika kukabidhi vitabu na kumbukumbu zote za ufilisi kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika ambaye atawajibika kuzitunza, na ndani ya miezi ishirini na minne (miaka miwili), Mrajis wa Vyama vya Ushirika atapeleka kumbukumbu hizo za ufilisi kwenye Ofisi ya kumbukumbu ya Taifa (Archives).

## SEHEMU YA SITA

## HITIMISHO

Ufilisi wa Vyama vya Ushirika vilivyofutwa umekuwa na changamoto nyingi ambazo zimesababisha zoezi la ufilisi kutokamilika kwa wakati. Changamoto hizo zinatokana na wafilisi wengi wa Vyama vya Ushirika kutokuwa na uelewewa wa kutosha kuhusu Sheria na taratibu zinazotakiwa kuzingatiwa katika utekelezaji wa jukumu hili na hivyo kuufanya ufilisi kuchukua muda mrefu.

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuondokana na changamoto hizo kwani utakuwa nyenzo muhimu katika kuwawezesha wafilisi wa Vyama vya Ushirika kufahamu wajibu na nafasi yao katika kukamilisha ufilisi. Hivyo, ni matumaini kuwa mwongozo huu utatumiwa na kusimamiwa ipasavyo na hatimaye kuwawezesha wafilisi kukamilisha Ufilisi kwa wakati muafaka kulingana na muda uliowekwa katika mwongozo huu, na kwa mujibu wa taratibu zilizopo, ili kuondoa changamoto iliyopo ya masuala ya ufilisi kuchukua muda mrefu.